|                                          |   |
|------------------------------------------|---|
| Sababu za kukamatwa .....                | 1 |
| Kumtambua anayekukamata.....             | 1 |
| Kumgusa ama kumfungia aliyekamatwa.....  | 1 |
| Matumizi ya nguvu wakati wakukamata..... | 1 |
| Haki ya kukimya.....                     | 1 |

### **MAMLAKA YA KUKAMATA**

|                                  |   |
|----------------------------------|---|
| Raia.....                        | 2 |
| Afisa mtekelezaji wa sheria..... | 2 |
| Chifu.....                       | 2 |
| Hakimu.....                      | 3 |
| Kibali cha Mahakama .....        | 3 |

### **UTARATIBU KATIKA KITUO CHA POLISI**

|                                                                  |   |
|------------------------------------------------------------------|---|
| Haki za kijumla unapozuliwa na polisi .....                      | 3 |
| Kumkagua aliyekamatwa .....                                      | 3 |
| Kufuatilia ulipo: Kunukuu kukamatwa .....                        | 3 |
| Alama za vidole na picha .....                                   | 3 |
| Taarifa .....                                                    | 3 |
| Kuwasiliana na wengine unapozuliwa katika kituo cha polisi ..... | 4 |
| Kutambuliwa katika waride .....                                  | 4 |

### **Uwezekano wa kuachiliwaa huru kutoka mikononi mwa polisi: bondi/ dhamana**

|                          |   |
|--------------------------|---|
| Ripoti za dakitari ..... | 4 |
| Mashitaka .....          | 4 |

### **MAWAIDHA UNAPOKAMATWA**

### **UTARATIBU MAHAKAMANI**

|                        |   |
|------------------------|---|
| Kujibu mashitaka ..... | 5 |
| Barua za mtajo .....   | 6 |

### **UPANDE WA MASHITAKA**

|                                                                    |           |
|--------------------------------------------------------------------|-----------|
| Uamuzi wakushitaki .....                                           | 6         |
| Uwezekanowa kuachiliwa huru kesi inapoendelea: bondi/dhamana ..... | 7         |
| <b>KUSIKIZWA KWA KESI MAHAKAMANI .....</b>                         | <b>7</b>  |
| Mudawa kusikizwa kwa kesi .....                                    | 8         |
| Kesi ya upande wa mashitaka .....                                  | 8         |
| Kesi ya Upande wa kupinga mashitaka .....                          | 9         |
| Kusujudia .....                                                    | 9         |
| <b>HUKUMU .....</b>                                                | <b>10</b> |
| <b>MAOMBI YA KUPUNGUZA ADHABU .....</b>                            | <b>10</b> |
| <b>KIFUNGO .....</b>                                               | <b>10</b> |
| Aina za vifungo .....                                              | 10        |
| <b>RUFAA .....</b>                                                 | <b>12</b> |
| <b>MAWAIDHA YA KUJIWAKILISHA MAHAKAMANI .....</b>                  | <b>13</b> |

# MWONGOZO WA KUJIWAKILISHA

## Utaratibu wa masuala ya jinai

Makosa ya jinai ni mgogoro wa umma. Katika maswala ya jinai, serikali inamshitaki aliyefanya makosa ya jinai kwa niaba ya umma. Hii ni tofauti na kesi za kiraia ambazo zinahusu watu binafsi ambapo, kwa mfano, mmoja wao anahitaji kufidhiwa na mwingine.

Utaratibu wa masuala ya jinai huanza mara unapokamatwa. Utaratibu huu unaendelea hadi unapopatikanaau kutopatikana na hatia. Unapopatikana na hatia, utaratibu huu unaweza kuendelea iwapo utakata rufaa.

## HAKI ZA ALIYEKAMATWA NA UTARATIBU WA KUKAMATWA

Hizi ndizo Haki zako unapokamatwa:

### Sababu za kukamatwa

- Anayekukamata sharti akufahamisha kiini cha kukukamata



## Kujitambulisha kwa anayekukamata

- Afisa anayekukamata sharti ajitambulishe kwa jina na cheo chake, na kwa uwazi lazima nambari yake ya kazi iwe katika sharti lake
- Kama afisa hajavaa sare zake rasmi, lazima akuonyeshe kitambulisho chake cha polisi
- Ikiwa unakamatwa na raia, hakimumu au chifu, lazima akufahamishwe kuwa yeye sio afisa wa polisi na kuwa anakupeleka kwa polisi

## Haki ya kufanyiwa utu

- Afisa wa polisi sharti akufanyie utu na heshima

## Kuguswa au Kuzuiliwa kwa mtuhumiwa



- Anayekukamata anaweza kukugusa, kukuzuilia au kukuweka pingu ikiwa unakataa kuwa mikononi mwake ama unapojaribu kutoroka

## **Matumizi ya Nguvu wakati wa kukamata**

- Afisa wa polisi anaweza kutumia nguvu za kadri anapokukamata ikiwa itahitajika kufanya hivyo. Lakini hafai kutumia nguvu ambazo zitasababisha kifo.
- Afisa wa polisi anaweza kutumia nguvu ikiwa:
  - Umeshitakiwa au kuhukumiwa kwa makosa ya jinai na unajaribu kutoroka
  - Ikiwa unatishia maisha ya afisa huyo kwa wakati huo
- Ikiwa afisa atatumia nguvu kupita kiasi, akusababishie majeraha au kukuua, atakuwa amefanya kosa la jinai. Wewe au jamaa zako wanaweza kumshitaki ili kuwepo na ridhaa.
  - Kwa mfano, itakuwa kinyume cha sheria ikiwa polisi atakuchapa hadi kukuumiza anapokukamata.

## **Haki ya kukimya**

- Ni sharti utoe jina na anwani yako unapokamatwa
- Haikulazimu kunena jambo lolote ambalo linaweza kutumika dhidi yako, kukiri au kusadiki makosa ya jinai. Haikulazimu kuandikisha taarifa au kusaidia polisi katika uchunguzi.

## **Haki ya Kutengwa Kizuizini**

- Ikiwa umekamatwa, unafaa kuzuiliwa kando na wanaotumikia

kifungo gerezani

- Waume wanafaa kuzuiliwa katika vyumba tofauti na vya wanawake
- Watato hawafai kuwekwa pamoja na watu wazima katika chumba kimoja. Wasichana wadogo wanafaa kuwekwa katika usimamizi wa afisa wa polisi wa kike.

## **Haki ya kuwasilishwa mahakamani haraka iwezekanavyo**

- Ikiwa hamna amri ya kukukamata, lazima upelekwe kwa hakimu bila kucheleweshwa au uachiliwe huru.
- Ikiwa kuna amri ya kukukamata, lazima upelekwe kotini kabla ya masaa 48 kukamilika au kabla ya siku 14 kukamilika ikiwa unashitakiwa na makosa kama ya mauaji, au wizi wa kimabavu
- Ukikamatwa siku ya likizo ya kitaifa au wikendi, lazima uletwe kotini siku ya kwanza ya kikazi inayofuata
- Ukikamatwa mbali na koti, lazima uletwe kotini haraka iwezekanavyo

\*\*\*\*Ukizuiliwa Kwakipindi kirefu kinyume na sheria, mfahamishe wakili wako haraka iwezekanavyo.

## **NANI ALIYE NA MAMLAKA YA KUKUKAMATA?**

### **Raia**

- Raia mwenzako anaweza kukukamata ikiwa:
  - Umefanya kosa kuu la jinai kama vile; wizi, mauaji, au kumuumiza mwingine
  - Umefanya kosa la jinai na polisi wanakutafuta
  - Umeharibu mali ya raia huyo



- Ikiwa raia atakukamata, lazima upelekwe kwa kituo cha polisi haraka iwezekanavyo

- Ikiwa hamna sababu kuu ya kukukamata, itabidi polisi wakuachilie huru
- Polisi wakithibitisha kuwa huenda umefanya kosa la jinai, wanaweza kukuzuilia hadi masaa 48 wakifanya uchunguzi
- Uchunguzi ukikamilika, polisi wanaweza kukushitaki au wakuachilie huru

### **Afisa mtekelezaji wa sheria**

- Afisa wa polisi ana mamlaka ya kukukamata ikiwa:
  - Umefanya au anashukiwa kufanya kosa la jinai
  - Unazuia utendakazi wake au uchunguzi anaoufanya
  - Unapojaribu kutoroka kutoka kizuizini
  - Ukiasi jeshi
  - Kuna kibali cha mahaka ukamatwe

### **Chifu**

- Chifu anaweza kukukamata ikiwa:
  - Unatuhumiwa kufanya au kupanga kufanya kosa la jinai
  - Kuna kibali cha mahakama ukamatwe
- Chifu akikukamata lazima upelekwe kwa polisi
- Chifu akikukamata ikiwa unatuhumiwa kufanya jambo fulani, lazima upelekwe kotini kabla ya masaa 12 au uachiliwe huru

### **Hakimu**

- Hakimu anaweza kukukamata ikiwa utafanya kosa la jinai ukiwa

mbele yake au katika mahali ampapo anatekeleza mamlaka yake ya kikazi

### **Kibali cha mahakama**

- Mahakama inawezakutoa kibali ukamatwe ikiwa:
  - Haujatimiza masharti ya bondi/dhamana uliyopewa
  - Haujajiwazilisha mbele ya mahakama inavyotakikana

## **UTARATIBU KATIKA KITUO CHA POLISI**

### **Haki za Kijumla ukiwa Kizuizini mwa Polisi**

- Una haki ya kupata chakula, malazi, usafi na afya njema
- Una haki ya kufahamishwa maamuzi yoyote yanayokuhusu
- Unahaki ya kuheshimiwa na dhidi ya kufanyiwa unyama

### **Ukaguzi wa aliyekamatwa**

- Ikiwa umekamatwa, polisi wanaweza kukukagua. Wanaweza kuchukua vilivyo vyako na kuvihifadi mahali salama. Polisi hawafai kuchukua viatu au mavazi yako
  - Lazima polisi wanukuu mali yako yote waliyohifadhi. Lazima udhibitishie na kutia sahihi. Polisi pia lazima watie sahihi.
  - Polisi wanaweza kuchukua na wasikurudishie silaha uliyokuwa nayo
- Ikiwa wewe ni mwanamke, polisi wa kike ndiye atakayekukagua pekee.

### **Kufuatilia uliko: Kunukuu Kukamatwa**

- Jina lako, anwani yako na sababu za kukamatwa zinafaa kunukuliwa


katika kitabu spesheli cha kunukuu mkasa (Occurrence Book) unapoingia katika kituo cha polisi

## Alama za Vidole na Picha

- Ukiwa katika kituo cha polisi, picha yako na alama za vidole zinaweza kuchukuliwa. Polisi wanaweza kutumia nguvu za kadiri kuchukua picha na alama za vidole ikiwa utakataa kuzitoa kwa hiari
- Polisi wanaweza kutumia alama za vidole:
  - Kubaini ikiwa umewahi kufanya kosa la jinai hapo wali
  - Kubaini ikiwa alama zako za vidole zinafanana na zile zilizopo mahali pa tukio la kosa la jinai unaloshukiwa kufanya
  - Kuhifadhi rekodi ya kosa la jinai unalotuhumiwa kufanya ikiwa utapatikana na hatia
  - Picha yako yaweza kutumika katika uchunguzi wa polisi. Kwa mfano, mhadhiriwa wa tendo la jinai anaweza kuonyeshwa picha yako imsaidie kutambua ikiwa ndiwe uliyemdhuru.

## Taarifa

- Kumbuka kuwa una **haki ya kukimya** (iliyoeleza hapo awali). Chochote utakachonena chaweza kutumiwa na polisi dhidi yako.
- Taarifa uchunguzi unapofanywa—bado haujashitakiwa kwa kosa la jinai
  - Afisa wa polisi atakuomba uandike taarifa ili kubaini ikiwa ulihusika na kosa la jinai
  - Afisa akiamini kuwa hukuhusika na kosala jinai lililotendeka, atakuachilia huru.



- Taarifa baada ya kushitakiwa
  - Kabla ya kutoa taarifa, afisa wa polisi lazima akufahamishe kuwa haikulazimu kutoa taarifa hiyo na ikiwa utaitoa, itakuwa kwa hiari na yaweza kutumiwa dhidi yako. Afisa wa polisi atakuomba uarifu kilichotendeka.
- Kuungama – kukubali kuwa una hatia ya kosa la jinai
  - Kuungama kunakofanywa kwa afisa wa polisi hakuwezi kubaliwa mbele ya mahakama. Afisa wa polisi hana sababu yoyote ya kukulazimu kuungama.
  - Mtu anaweza kuungama mahakamani, mbele ya hakim au jaji pekee. Kuungama huku ndiko kunakokubalika na kuchukuliwa kama wa ukweli.

## **Kuwasiliana na wengine ukizuiliwa katika Kituo cha Polisi**

- Ukikamatwa, unahaki ya kumpigia jamaa, rafiki au wakili simu - mara moja pekee
- Ukiwa kizuizini, wakili wako anaweza kukutembelea awezavyo. Jamaa au rafiki anaweza kukutembelea kizuizini kati ya saa kumi na mbili asubuhi hadi saa kumi na mbili jioni pekee – chini ya uangalifu wa afisa wa polisi.

## **Kutambuliwa katika waride**

- Waride hii inamsaidia aliyeshuhudia kosa la jinai kudhibitisha kuwa wewe ndiye aliyeona ukifanya kosa hilo.
- Uamuzi ni wako ikiwa ungependa kuwa katika waride hiyo
- Ukiamua kuwa katika waride hiyo, lazima wawepo watu 7 pia – wakipungua. Watu hawa inabidi wakaribie kufanana nawe iwezekanavyo.

## **Uwezekano wa kuachiliwa kabla ya kupelekwa mahakamani**

- Bondi ni njia mojawapo ambayo unaweza kuachiliwa kutoka kizuizini mwa polisi kabla ya kupelekwa mahakamani
- Ikiwa hatia uliyoshukiwa kufanya sio kubwa, unaweza kuachiliwa kutoka kituo cha polisi kwa kutoa amana ya pesa taslimu au kuahidi kuwa utaenda kotini au utarudu katika kituo cha polisi kwa tarehe/masaa yaliliyowekwa.
  - Tazama kipengee cha “bondi/dhamana” kilichomo hapa chini kwa ufahamu zaidi.

## **Ripoti ya Daktari**

Ripoti ya daktari inaweza kutumika kwasababu zifuatazo:

- Kubaini uwezekano kuwa ulifanya kosa la jinai.
  - Kwa mfano, ikiwa mtuhumiwa aliumia akifanya kosa la jinai, na hauna majeraha, kuna uwezekano kuwa mtuhumiwa huyo sio wewe.
- Kubaini umri wako.
  - Lazima uwe na umri wa zaidi ya miaka minane ili ushitakiwe kwa kosa la jinai.
  - Ikiwa una umri wa kati ya miaka 8 na 18, unatambuliwa kisheria kuwa mtoto na unafaa kushitakiwa katika mahakama ya watoto. Pia, huwezi kuhukumiwa kifo iwapo utapatikana na hatia.
- Kubaini hali yako ya akili
  - Lazima ibainike kuwa ulikuwa wa akili timamu wakati unatuhumiwa ulifanya kosa la jinai
  - Pia, lazima uwe wa akili timamu wakati kesi yako inaposikizwa. Jambo hili ni muhimu kwa sababu unafaa kuelewa yanayoendelea mahakamani.
  - Sheria inatambua kuwa watu wote wana akili timamu wanapofanya makosa ya jinai hadi kutokananaushahidi wa ripoti za daktari itambulike kuwa sivyo.


## **Mashitaka**

- Kwa lugha iliyo wazi, shitaka ni kosa la jinai unalotuhumiwa kufanya. Shitaka linajumlisha:
  - Sheria: Shitaka lazima litaje sheria unayotuhumiwa kukiuka. Ikiwa hamna sheria uliyokiukwa, basi hamna kosa la jinai ulilofanya.
  - Vipengee vya hatia: tarehe, wakatina mahali unapotuhumiwa kufanya kosa la jinai, na matukio ya kweli ya kosa la jinai lililofanyika.

- Shitaka hukusaidida kufahamu na kuelewa fika kesi dhidi yako ili uweze kujitetea.

## MAWAIDHA IKIWA UNAKAMATWA NA KUPELEKWA KATIKA KITUO CHA POLISI

- Tulia na usijaribu kuzuia kukamatwa
- Toa jina lako, anwani na habari yoyote inayokutambulisha, na fahamisha ikwa una chini ya umri wa miaka 18.
- Kuwa mpole unapowasiliana na afisa wa polisi
- Omba jamaa wako au rafiki afahamishwe kuwa umekamatwa, ili awe katika kituo cha polisi.
- Omba umpigie simu jamaa, rafiki au wakili wako
- Usiandike wala kutia sahihi makubaliano yoyote yaliyoandikwa



- Usiungame kwa jambo lolote ambalo hujatenda
- Nukuu

## UTARATIBU MAHAKAMANI

### Kujibu Mashitaka

- Ukishitakiwa kwa kosa la jinai unaletwa mbele ya mahakama. Utasomewa mashitaka nakina cha kosa. Utajibu kwa kukiri mashitaka au kukataa kwa kusema “ndio” au “la”. – huku ndiko kujibu mashitaka. Ukikiri kwa kusema “ndio” unamaanisha kuwa ulifanya kosa la jinai uliloshitakiwa nalo. Kujibu mashitaka kwa kukana “la” ni unamaanisha kuwa hukufanya kosa la jinai unalotuhumiwa kufanya. Chochote unachonena mahakamani kinanukuliwa.
- Lazima uwe na uwezo wa kufahamu kinachoendelea mahakamani. Mahakama yaweza kuzungumzakwa lugha ya Kingereza au Kiswahili. Ikiwa huelewi lugha hizi, mahakama itakupa mkalimani bila malipo.
- Ikiwa utakana mashitaka kwa kusema “la”, utapewa tarehe ambayo lazima utarudi mahakamanikesi isikizwe. Kusikizwa kwa kesi kutabaini kuwa unahatia au huna hatia ya mashitaka dhidi yako.
  - Ukipewa bondi/dhamana, lazima urudi mahakamani mwenyewe tarehe uliyopewa. Ikiwa hutarudi, mahakama itatoa kibaliukamatwe.
  - Ikiwa hutapewa bondi/dhamana, itabidi uwe kizuizinihadi kesi yako isikizwe
- Ukikiri kosa lako kwa kusema “ndio”, umekubali kuwa ulifanya kosa la jinai. Wakili anayeshitaki atasoma matukio ya kweli ya kosa la jinai.
  - Ikiwa hutakana matukio hayo, mahakama itabaini kuwa una hatiana utaadhibiwa vilivyo. Adhabu itakuwa kifungo.



- Ikiwa si wazi kuwa unakiri au kukataa kwasababu hukubaliani na matukio ya kweliyaliosomwa au kukana kuwa na hatia, basi lazima mahakama ibadili jibu la mashitaka yako na kuwa “la”.

## Barua za mtajo

- Mahakama hutoa baruaza mtajo zinazohakikisha kuwa upo katika mamlaka ya mahakama
- Ikiwa uliachiliwa kwabondi/dhamana, mtajo wa kesi yako utatumwa kila baada ya siku 30 baada ya kuitikia kesi, hadi kusikizwa kwa kesi yako kukamilike.
- Ikiwa uko gerezani, mtajo wa kesi yako utatumwa kila baada ya siku 14 -baada ya kuitikia kesi yako. Unapewa nafasi ya:
  - Kuomba dhamana yako ipunguzwe hivi kwamba uachiliwe kutoka gerezani wakati kesi yako inasikizwa
  - Kuomba wakili wako au wewe mwenyewe upewe taarifa za mashahidi
  - Kuomba uchukuliwe hospitalini ikiwa wewe ni mgonjwa
  - Kabadili ulivyojibu au kuitikia mashitaka
  - Kuomba kesi yako isikizwe

## UPANDE WA MASHITAKA

Ukikana mashitaka kwa kusema “la”, kesi itasikizwa. Katika kusikizwa kwa kesi kuna pande mbili: **a)** upande wa mashitaka **b)** upande wa kupinga mashitaka/ wa kujitetea (wewe, mtuhumiwa). Upande wa mashitaka una jukumu la kuhakikisha kuwa mahakama inafahamu matukio halisi na utajaribu kudhibitisha kuwa ulifanya kosa la jinai. Pande zote mbili zitatoa ushahidi na kuita mashahidi. Baada ya matukio ya kwelikuwasilishwa, hakimu au jaji atatoa uamuzi kutokana na matukio hayo na ufahamu wake wa sheria.

➤ Anagalia “utaratibu wa kusikizwa kwa kesi” katika sehemu iliyopo hapa chini kwa ufahamu zaidi.

Inalazimu upande wa mashitaka kufanya mambo yote kwa haki. Kwa kawaida serikali ndiyo upande wa mashitaka na husimamia maswala ya jinai. Nchini Kenya, hili ni jukumu la Kaimu Mkurugenzi wa mashitaka ya umma (DPP)– kitengo cha afisi ya Mwanasheria Mkuu (AG). Lakini, ikiwa serikali haitilii maanani kesi, watu binafsi wanaweza kushitaki au waombwe na serikali kushitaki kwa niaba ya serikali.

### **Uamuzi wa kushitaki unategemea mambo mengi:**

**1) Lazima kuwepo na ushahidi wa kutosha.** Upande wa mashitaka utaangalia ushahidi wote uliopo na kuamua ikiwa kuna ushahidi wa kutosha utakao dhibitisha mashitaka. Ikiwa hamna ushahidi wa kutosha, mashitaka yatatupiliwa mbali au kutolewa.

**2) Ikiwa kosa la jinai ni zito.** Hii inategemea namatukio yanayozunguka kosa, na hata hali ya kosa la jinai yenyewe. Ikiwa upande wa mashitaka utaonelea kuwa lalamiko ni duni au hafifu au limetokana na uhasama wa kibinafsi, huenda utakataa kushitaki

**3) Ikiwa afya yako imedhoofika au unaugua ugonjwa waakili,** upande wa mashitaka unaweza kuamua kutoendeleza kesi. Ikiwa una akili punguani, upande wa mashitaka unaweza kuendeleza kesi iwapo utadhibitisha kutoka kwa mhudumu wa afya kuwa uko wa hali nzuri ya afya na kuwa mwanasheria mkuu ametoa hakikisho, kisheria,kuwa kesi iendelee.


**4) Msukumo/nia ya malalamishipia** huzingatiwa haswa katika kesi za jinai zilizo na uzito. Upande wa mashitaka unahitaji ushahidi wa malalamishi. Ikiwa upande wa mashitaka unahisi kuwa malalamishi hayaambatani na kesi, upande huo hautapendelea kushitaki kesi hiyo.

**5) Lazima ushitakiwe katika eneo la tukio la kosa.** Hili linafaamika kamaeneo la mamlaka ya mahakama. Tendo lazima lifanyike nchini Kenya au liwe na uhusiano na Kenya ili lishitakiwe au kuchunguzwa na mahakama za Kenya. Hivi ni vizuizi vya mahakama za mahakimu

kulingana na aina za hukumu na faini zinazoweza kutoa au kuweka. Mahakama za juu hazina vizuizi hivi katika mamlaka yao.

## Uwezekano wa Kuachiliwa kwa Mshukiwa Kesi inaposikizwa: Bondi/Dhamana

**Dhamanani** amri ya mahakama uachiliwe kwa muda kesi inaposikilizwa. Hii niwa maelewano kuwa lazima urudi mahakamani kesi yako inaposikizwa au kutajwa. Ikiwa utapewa dhamana ya pesa taslimu, utahitajika kuweka amana ya kiwango fulani cha pesa katika ofisi ya usajili ya mahakama. Ikiwa utarudi mahakamani siku zote unazohitajika, utarudishiwa pesa hizi hata kama utapatikana na hatia ya kosa uliloshitakiwa.



**Bondi** ni sawia na amri lakini inahusu kesi ndogo za jinai na haihusu pesa kwa mara hiyo. Bondi inakuhitaji kuahidi kwa maandishi kuwa iwapo hutarudi mahakamani, utalipa kiwango fulani cha pesa. Lazima uonyeshe nakudhibitishia mahakama kuwa una uwezo wa kulipa pesa ulizoahidi au kitu kilicho na kiwango sawia (kwa mfano: hati miliki ya shamba, na thibitisho za malipo ya mshahara wako, nakadhalika)

Unaweza kuomba uachiliwekwa dhamana unapozuliwa katika kituo cha polisi au mara unapofika mahakamani. Kijumla, una haki ya kikatiba kuachiliwa kwa dhamana hadi kesi yako iamuliwe na mahakama. Lakini, maombi ya kuachiliwa kwa dhamana yanaweza kukatiliwa iwapo:

- Kosa la jinai ni la uzito au sugu (kama mauaji, kuasi au wizi wa kimabavu)
- Huna anuani ya kudumu – mahali unapokaa
- Mahakama ua polisi wanaamini kuwa kuna uwezekano mkubwa kuwa utatoroka
- Umekosa kurudi mahakamani hapo awali
- Inaaminika kuwa wewe ni tishio kwa usalama wa taifa au kwa mashahidi

Ikiwa umewahi kuachiliwa kwa dhamana na haukuzingatia masharti yaliyowekwa na mahakama, dhamana yako yaweza kufutiliwa mbali na uamrishwe kulipa pesa au ufungwe gerezani.

## **KUSIKIZWA KWA KESI**

Unachukuliwa kuwa asiye na hatia hadi ukubali Mashitaka au mahakama iliyo na mamlaka ya kusikiza kesi didhi yako ikupate na hatia.

- Katika mwanzo wa kusikizwa kwa kesi didhi yako, utasomewa mashitaka. Mashitaka yapo katika notisi rasmi kuhusu kosa la jinai unalotuhumiwa kufanya.
- Kwa wakati huu, unaweza kubadili mwendaji wako wa kukiri kulifanya kosa au kukataa. Ikiwa mwendaji wako haubadili, kesi

yaweza anza kusikizwa.

- **Kabla ya kesi kuanza kusikizwa, yafaa ujitayarishe na yafuatayo:**
  1. Vitu vyote utakavyovitumia katika kujitetea
  2. Ikiwa huelewi Kingereza au Kiswahili, unaitaji kuomba upewe mkalimani kwa mapema. Wakalimani hutolewa na mahakama bila malipo.
  3. Ni haki yako kuwa na taarifa za upande wa mashitaka na maswali utakayouliza mashahidi wa upande wa mashitaka, ili ujitayarishe kwa kesi. Unafaa kuitisha vitu hivi haraka iwezekanavyo.
- Ni muhimu wazazi au wanaowatunza watoto walioshitakiwa wawe mahakani kila wakati kesi inaposikizwa



## Muda wa Kesi Kusikizwa

Mtu yeyote aliyeshitakiwa kwa kosa la jinai sharti kesi didhi yake isikizwe inavyostahili na kwa muda unaofaa. Haya huwa hayafanyiki sababu ya uchunguzi duni, kukosa kwa mashahidi wa upande wa mashitaka, na kuwepo na upungufu wa wafanyakazi katika idara ya mahakama, nakadhalika.

- Kwa jumla, muda uliowekwa haufuatiwi kwa makini na mahakama hutoa sababu nyingi za kuhairisha kusikizwa kwa kesi.
- Wewe (mshatikwa) au upande wa mashitaka unaweza kuomba mahakama ihairishe kesi wakati wowote inaposikizwa. Kwa mfano, kesi inaweza kuhairishwa ikiwa wewe ni mgonjwa.
- Ni muhimu kuwa kuhairishwa kwa kesi hakutumiwi vibaya ama kama mbinu ya kuchelewesha kesi kwa lengo la kukuadhibu. Ukishuku hili linafanyika, unaweza kuomba mahakama isikubali ombi la kuhairisha kesi na uombe kesi itupiliwe mbali. Ni sharti mahakama iamue mwelekeo wa kesi baada ya haya.
  - Ikiwa ungali unangoja kukamilika kwa kusikizwa kwa kesi didhi yako, na umekuwa kizuizini kwa muda mrefu zaidi ya hukumu inayokubalika kisheria, wafaa kufahamisha mahakama kuhusu hili jambo. Kwa mfano, ikiwa umekuwa kizuizini zaidi ya mwaka mmoja, lakini kosa la jinai unalotuhumiwa kulifanya huwa na adhabu ya kifungo cha miezi sita, inafaa ufahamishe mahakama kuhusu jambo hili.

## Muda uliowekwa kwa Kesi didhi ya Watoto

- Kulingana na sheria ya bunge kuhusu watoto ya mwaka wa 2001, kesi dhidi ya watoto inafaa kuchukua muda usiozidi miezi 3 kutoka wakati mwikio wa kukiri au kukataa kesi unapofanywa hadi kukamilishwa na kama sivyo kesi itupiliwe mbali.
- Kwa kesi zilizo katika mahakama ya juu au ile ya rufaa, kesi hizi zafaa kusikizwa kwa muda usiozidi miezi 12 na kwa wakati huo mtoto hafai kuwa kizuizini kwa zaidi ya miezi 6 bila kuachiliwa kwa dhamana.

## **Kesi ya Upande wa Mashitaka**

Ni jukumu la upande wa mashitaka kudhathimini bila tashwishi yoyote kuwa ulifanya kosa la jinai unalotuhumiwa kulifanya. Upande wa mashitaka utatoa ushahidi kudhathimini kesi kwa kuita mashahidi. Huu ndio mpangilio wa kesi ya upande wa mashitaka:

### **1. Upande wa mashitaka kutoa ushahidi didhi yako.**

Upande wa mashitaka unaweza kuita mashahidi kueleza matukio ya kesi mahakamani

### **2. Uchunguzi**

Shahidi ataitwa kizimbani na atatakiwa ahaidi kueleza kwa ukweli. Atafanya hili kwa kuhapa. Upande wa mashitaka utaendelea kwa kuuliza maswali ili kupata ujumbe kutoka kwa shahidi kuhusu matukio ya kosa la jinai unalotuhumiwa kufanywa.

### **3. Kuhojiwa**

Huu ndio wakati wa kuuliza shahidi wa upande wa mashitaka maswali kama haki yako. Maswali yako yanafaaya jaribu kuonyesha/kufahamisha mahakama kuwa shahidi hawezi kuaminika au kuwa shahidi hana ufahamu wa matukio. Maswali haya sharti yahusu maswala yaliyozungumziwa wakati wa uchunguzi

### **4. Kuchunguza tena**

Upande wa mashitaka unakubaliwa kuuliza maswali zaidi yanayolenga kufafanua au kutilia mkazo maswala yaliyoleta utata wakati wa uchunguzi.

### **5. Uamuzi wa Mahakama**

Mwishoni mwa kesi ya upande wa mashitaka, na ikiwa ushahidi uliotolewa na upande wa mashitaka dhidi yako unatosha, hakimu au jaji ataamua kuwa una kesi ya kujibu. Utahitajika kujibu (angalia sehemu ya kujitetea iliyopo hapa chini kwa ufahamu zaidi). Ikiwa hamna ushahidi wa kutosha, mahakama itaamua kuwa hamna kesi ya kujibu na utaachiliwa huru kuusu mashitaka dhidi yako bila masharti yoyote.



**Wakati wowote na kabla ya uamuzi wa mahakama, upande wa mashitaka unaweza kusimamisha kesi na uachiliwe huru.** Hili haliwezi kuzuia kutoshitakiwa tena ikiwa maafisa wa polisi watapata ushahidi mpya na wenye nguvu dhidi yako. Lakini, ikiwa umeachilwa huru, hauwezi kushitakiwa tena kwa kosa na matukio yale yale hata kwa ushahidi huo mpya. Kesi itakuwa imekamili. Sharti rufaa ikatwe kupinga kuachiliwa huru. (Tazama upande wa Kukata Rufaa hapa chini kwa ufahamu zaidi)

### **Kesi ya Upande wa Kupinga Mashitaka/Kujitetea**

Mahakama ikiamua kuwa una kesi ya kujibu, una haki ya kujitetea na kuita mashahidi. Mpangilio ni sawia na ule wa upande wa mashitaka (tazama “Kesi ya Upande wa Mashitaka” hapa juu). Utauliza maswali wakati wa uchunguzi na baada ya hayo upande wa mashitaka una nafasi ya kukuhoji. Pia utakuwa na nafasi ya kuchunguza tena. Hata ikiwa hautaita mashahidi, mahakama itataka kusikiza matukio ya kosa unalotuhumiwa kufanya kutoka kwako.

### **Kulingana na hali ya Kesi, unaweza kuamua:**

- 1) **Kukimya:** Wakati mwingine, unaweza kukosa la ziada kueleza mahakama. Katika baadhi ya kesi, kueleza mahakama zaidi kwaweza kufanya kujiteteakwako kuwe hafifu. Ikiwa huelezei zaidi, haimaanishi kuwa unakubaliana na upande wa mashitaka. Lakini, mahakama inakusudia uongee.
- 2) **Kutoa ushahidi bila kula kihapo.** Ukitoa ushahidi bila kula kihapo, hauahidi kusema ukweli. Hili laweza kuwafanya watu wachukulie unayoyasema kama yasiyo ya ukweli.
- 3) **Kutoa ushahidi chini ya kihapo:** Ukitoa ushahidi baada ya kula kihapo, hii inamaanisha kuwa unahaidi kuwa mkweli unapoarifu mahakama na hata unapojibu maswali mahakamani. Lakini, iwapo utahaidi kuwa mkweli na ugunduliwe kuwa mdanganyifu, utapatikana na hatia ya kusema uwongo, kosa ambalo unaweza kuhukumiwa kifungo cha miezi sita gerezeni.



## Kusujudia

Baada ya upande wa mashitaka na ule wa kujitetea kutoa ushahidi wao na kukamilisha kesi zao, kila upande, kuanzia na ule wa mashitaka, una nafasi ya kutoa ushahidi wao kwa ufupi kwa maandishi au kwa kunena. Huku ndiko kusujudia. Upande wa mashitaka utajaribu kufahamisha mahakama kuwa umebaini bila tashwishi yeyote kuwa mshitakiwa amefanya kosa. Wewe, kama upande wa kujitetea, utajaribu kuonyesha kuwa ushahidi uliotolewa dhidi yako hauna nguvu kudhibitisha kuwa una hatia. **Kesi za kihistoria** ambazo zimeamuliwa na mahakama kwa maswala sawia au hatia sawa hutumika kama mifano wakati wa kusujudu ili kushawishi hakimu au jaji kuegemea upande wako.



## HUKUMU

Hukumu ni uamuzi wa mwisho wa hakimu au jaji kuhusu kesi kulingana na maelezo halisi yaliyotolewa mahakamani na sheria inayoambatana.

- Utaambiwa ikiwa umepatikana na hatia au la kwa kosa la jinai ulilotuhumiwa kufanya
- Ikiwa hutapatikana na hatia, utaachiliwa huru.

## MAOMBI YA KUPUNGUZIWA ADHABU

Huku ni kumpa fursa mtu aliyepatwa na hatia kuelezea hali yake na kuomba hakimu au jaji kumpunguzia adhabu.

- Maombi haya hufanyika kabla ya jaji au hakimu hajatoa hukumu
- Kama mtu aliyepatwa na hatia, sharti upewe fursa ya kuomba kupunguziwa adhabu
- Maombi haya hufanyika mara tu unapopatwa na hatia
- Hufai kupinga kuwa huna hatia bali uombe kuhurumiwa
- Hutalazimishwa kunena lolote ikiwa utaamua kutotoa ombi hili.
- Kwa kesi zinazohusu watoto, kwa mujibu wa sheria watoto hawa wanapo fungwa, mahakama lazima izingatie yale yaliyo bora kwa mtoto husika.

**Kuna sababu kadha ambazo mahakama yaweza kuzingatia kufanya uamuzi wa kuhurumia nakutoa kifungo chepesi:**

- Ikiwa hiyo ndiyo mara yako ya kwanza kufanya kosa la jinai
- Ikiwa wewe ndiwe wa pekee unayetegemegwa/uliyeajiriwa nyumbani
- Ikiwa umejutia kosa lako
- Ikiwa hukuifaamu sheria kuhusu kosa lako

- Kosa lilikuwa la kiufundi
- Kuna mambo kando na uwezo wako kama, kulazimishwa, kutishwa, ama ulevi wakati ulipokuwa ukifanya kosa la jinai ambayo yalikusukuma hivi kwamba hungeweza kuyazuia

## KIFUNGO

Kifungo ni adhabu inayotolewa kwa kosa la jinai lililofanywa. Kwa mujibu wa sheria, kuna aina za vifungo kwa makosa tofauti na jaji au hakimumu sharti azingatie masharti haya.

### Aina za vifungo:

1. Mahakama inakupa fursa ya kwenda nyumbani ikiwa utahaidi kuzingatia masharti na ikiwa hutafanya kosa lolote la jinai au ikiwa hutaroka mahali hapo. Utapatiwa afisa wamajaribio na ni sharti ushirikiane na afisa huyo na kuzingatia mwelekeo atakaokupa la sivyo utapewa kifungo kikali.
2. **Amri ya Kufanya kazi kwa jamii** yaweza kutolewa dhidi yako ili ufanye kazi kama za usafi, kuokota takataka katika jamii kwa muda fulani. Kifungo hiki kinastahili waliopatwa na hatia ya makosa madogo madogo ya jinai
3. **Faini** ni amri ya mahakama inayokuitaji kulipa kiwango fulani cha pesa kama adhabu. Mahakama yaweza kuamuru faini hiyo iwe fidia kwa mhadhiriwa wa kesi. Usipolipa, utatiwa gerezeni hadi ufanye malipo.

Katika kesi za wizi au unyanganyi naikiwa ulichukua mali ya mhadhiriwa, utaamrisha kurudisha mali hayo kwa serikali ambayo itampa mhadhiriwa.

4. **Kifungo gerezeni** dhidi yako chaweza kuwa cha muda fulani au cha maisha. Kwa mujibu wa sheria, kuna muda usiozidi wa kufungwa gerezeni kwa makosa ya jinai fulani. Ni uamuzi wa hakimumu au jaji ikiwa utapewa kifungo hicho kisichozidi au la. Kifungo gerezeni chaweza amriwa kikiambatana na faini au faini badala ya kifungo gerezeni.

Kulingana na sheria ya bunge kuhusu watoto ya mwaka wa 2001, watoto waliopatwa na hatia na wenye umri chini ya miaka 16 hupelekwa katika shule ya urekebishaji ambayo hutoa mafunzo ya kielimu, kiufundi na ukulima. Kulingana na hali ya kesi, mahakama sharti iamue ikiwa ni chaguo bora kwa mtoto huyo.

## Vifungo Gerezani

### Kutumikia vifungo tofauti kwa wakati mmoja na vifungo mtawalia

Unaposhitakiwa na zaidi ya kosa moja katika kesi moja au unapopatikana na hatia na kuhukumiwa kwa makosa tofauti, vifungo tofauti kwa wakati mmoja au vifungo mtawalia hutolewa.

- **Vifungo tofauti kwa wakati mmoja.** Kwa mfano, ikiwa kifungo cha kwanza ni cha miaka 5 na cha pili ni cha miaka 7, kwa jumla vifungo hivi vyote ni vya miaka 7.
- **Kifungo mtawalia** ni kile ambacho unatumikiakifungo kimoja baada ya kingine, na kwa jumla utakuwa umetumikia vifungo vyote. Kwa mfano, ukihukumiwa kifungo cha miaka 7 kwa shitaka moja na kifungo cha miaka 10 kwa shitaka la pili, utatumikia kifungo cha jumla ya miaka 17 gerezani.

## Msamaha

Msamaha hutolewa kufupisha muda wa kifungo kutokana na maadhilifu mema.

- Kwa mujibu wa sheria ya bunge ya magereza, yeyote aliyehukumiwa ana haki ya msamaha kwa kiwango cha thuluthi ya kifungo chake gerezani. Kwa mfano, yeyote aliyehukumiwa kwa miaka 9 anaweza kutumikia miaka 6 pekee gerezani.
- Ili uwe na haki ya msamaha, sharti uwe unatumikia kifungo zaidi ya mwezi 1 na sharti uwe tayari umetumikia zaidi ya mwezi mmoja.
- Ikiwa utakosa ukiwa gerezani, unaweza kupoteza haki yako ya msamaha. Ingawa, utapewa haki ya kusikizwa kabla ya kupoteza haki hii.

- Ukipatikana na hatia kwa makosa fulani ambayo yana hukumu ya kifungo cha maisha gerezani (mauaji, wizi wa kimabavu nakadhalika) au ukifungwa gerezani kwa hiari ya Rais, hutakuwa na haki ya msamaha.

## **Kutangua Kifungo**

Hii ni ile hali ambayo mahakama inachelewesha kutoa hukumu ya kifungo. Hili hufanyika ikiwa mahakama inangoja uamuzi kutoka kwa mahakama nyingine kuhusu rufaa iliyokatwa (tazama sehemu ya rufaa hapa chini). Ikiwa rufaa itatupiliwa mbali, hukumu ya kifungo halisia itanza na utatumikia kifungo chote. Mahakama haitajumlisha muda ambao kifungo kilikuwa kimetanguliwa kama muda wa kifungo ulichotumikia.

## **Hukumu ya Kifungo cha Mashaushi (Corporal)**

Hukumu ya kifungo hichi ni ya kuchapwa kwenye sehemu za makalio. Hukumu ya kifungo cha mashaushi kimefutuliwa mbali na sheria za Kenya za hivi punde.

## **Kazi Ngumu**

Kuna baadhi ya hali, mahakama yaweza kuamuru kuwa - mbali na muda wa kutumikia kifungo gerezani, lazima ufanye kazi ngumu. Hili kwa kawaida hufanyika mahakama inapohisi kuwa kifungo chako chafaa kuwa zaidi ya hukumu iliyotolewa na sheria, haswa ikiwa kitendo chako kilikuwa cha kinyama au cha machukizo.

## **Hukumu ya Kifo**

Unaposhitakiwa na kupatikana na hatia ya mauaji, kuasi nchi, wizi wa kimabavu au kujaribu kuiba kimabavu, mahakama yaweza kuamuru uhukumiwe kifo.

- Kwa mujibu wa sheria za Kenya, jinsi ya kuwezesha hukumu hii ni kunyongwa shingoni hadi kufa
- Hukumu ya kifo haiwezi kuamrisha dhidi ya mtu aliye na umri chini ya miaka 18 wakati wa tendo la kosa la jinai.
- Hukumu ya kifo haiwezi kutolewa kwa mama mja mzito



- Tangu mwaka wa 1987, serikali ya Kenya haijawahi kutekeleza hukumu ya kifo kupitia kwa mahakama. Kenya imetia sahihi makubaliano ya kusitisha kwa muda kifungo cha hukumu ya kifo, ingawa idadi ya wanaohukumiwa kifo inazidi kuongezeka.
- Sharti Rais atie sahihi kibali cha kutekeleza hukumu ya kifo ndiposa hukumu hiyo itekelezwe.
- Rais ana mamlaka ya kukusamehe au kukupunguzia hukumu ya kifo na anaweza kuamuru uachiliwe au abadilishe hukumu ya kifo hadi ile ya maisha.

## RUFAA

Ukipatikana na hatia ya kosa la jinai, una haki ya kukata rufaa dhidi ya uamuzi kuwa una hatia au dhidi ya hukumu iliyotolewa. Ukikubali mashitaka, unaweza kukata rufaa kuhusu hukumu iliyotolewa, bali sio uamuzi kuwa una hatia.

- **Jinsi ya Kukata Rufaa**

- Una muda wa **usiku 14 baada ya uamuzi kutolewa kuwa una hatia** wa kukata rufaa. Usipokata rufaa kwa muda huu, itakulazimu kuipa mahakama sababu zitakazoshawishi ukieleza ni kwa nini hukukata rufaa. La sivyo rufaa yako haitakubaliwa mahakamani.
- Ikiwa utakosa feda za kukata rufaa, uneweza kukata rufaa kama **Kibapara**.
- Sharti utayarishe **Uombi wa Kukata Rufaa**. Stakabadhi hizi hutaja sababu za kukata rufaa. Hakikisha kuwa sababu zote umeziweka mle ndani, kwa kuwa zile zilizotajwa pekee ndizo zitakazozungumziwa wakati rufaa itakaposikizwa.
- Hakikisha kuwa uombi huo unajumlisha mashitaka dhidi yako, hatua za kesi mahakamani na uamuzi wa mahakama.
- Ikiwa upo gerezani, afisa wa zamu katika gereza hilo anaweza kukusaidia kukata rufaa kupitia kwa afisi ya usajili wa mahakama.

- **Mahakama za rufaa**

- Ikiwa umepatwa na hatia na hakimu katika mahakama za chini, utakata rufaa kwa mahakama kuu
- Ikiwa umepatwa na hatia na mahakama kuu, utakata rufaa kwa mahakama ya rufaa
- Kwa mujibu wa Katiba ya Kenya, unaweza kukata rufaa

kwa mahakama ya juu zaidi ikiwa ni jambo lenye umuhimu na linalohusu umma kwa jumla.

- Huwezi kukata rufaa zaidi ya hapa.

- **Kusikizwa kwa Rufaa**

- Mashahidi hawahusiki katika kusikizwa kwa rufaa. Ushahidi wa awali unapitiwa na hoja zako na za upande wa mashitaka zinasikizwa. Ushahidi mpya unaweza kubalika ikiwa mahakama itaonelea kuwa ni wa muhimu.
- Mahakama itatoa uamuzi kuwa;
  - Inakubaliana kuwa una hatia na itekeleze uamuzi huo, au
  - Huna hatia na ivutilie mbali uamuzi wa kupatikana na hatia
  - Inapunguza, kuongeza au kubadili hukumu dhidi yako
  - Inaamuru kesi yako isikizwe upya

- **Rufaa za waliopatwa na hatia lakini wasio na akili timamu**

- Ukipatikana na hatia lakini huna akili timamu, unaweza kuzuiliwa bila kupewa tarehe ya kuachiliwa. Hii ni kumaanisha kuwa unaweza kuzuiliwa kwa muda mrefu, au milele. Huwezi kuachiliwa hadi dakitari atangaze kuwa hali yako ni njema.
- Unaweza kukata rufaa dhidi ya uamuzi kuwa huna akili timamu, hivi kwamba upewe tarehe ya hakika ya kuachiliwa.

- **Dhamana unaposubiri Rufaa**

- Iwapo umepatikana na hatia na unakata rufaa, unaweza kuomba uachiliwe kwa dhamana ukingoja kusikizwa kwa rufaa



- Ikiwa mahakama za chini hazitakuachilia kwa dhamana, unaweza kupeleka ombi lako kwa mahakama ya juu.
- Kuachiliwa kwa dhamana kunategemea ikiwa kuna uwezekano kuwa utapatikana kuwa hauna hatia rufaa itakaposikizwa. Ikiwa kuna uwezekano kuwa utapatikana na hatia, au mahakama imewahi kukataa kukuachilia kwa dhamana hapo awali, utanyimwa dhamana kwa woga kuwa utatoroka.

## MAWAIDHAYAKUJIWAKILISHAMAHAKAMANI

- **Onyesha hisia nzuri.** Kuwa ndani ya mavazi safina yaliyo nadhifu. Hii itaonyesha mahakama kuwa unahieshimu na unajali kuhusu kesi yako
- **Kuwa mwenye heshima.** Heshimu kila mmoja aliye mahakamani. Usikatize hakimu/jaji anapozungumza. Unachokifanya ni muhimu sawia na unavyoonekana
- **Fika mahakamani mapema.** Ikiwa kesi yako inasikizwa wakati wa asubuhi, fika mahakamani kabla ya saa mbili za asubuhi. Ikiwa kesi yako inasikizwa wakati wa alasiri, fika mahakamani kabla ya saa nane za alasiri. Fahamisha Karani wa mahakama kuwa umewasili. Ukichelewa, kesi yako itahairishwa au itupiliwe mbali. Ukikosa kufika mahakani, unaweza kupigwa faini au ufungwe gereza.
- **Fahamu unalotaka kuuliza.** Uliza wafanyakazi wa mahakama kuhusu utaratibu na aina ya ujumbe wa kujaza katika fomu. Hawatakuambia unachotakikana kuandika katika fomu wala utakachosema kesi itakaposikizwa. Usaidizi huu unaweza kuupata kwawakili au mwanasheria.
- **Jiandae kabla ya kuja mahakamani.** Hakikisha kuwa una stakabadhi zote kesi inaposikizwana uje na nakala zinazohitajika. Wakumbushe mashahidi wako waje mahakamani kwa wakati unaostahili. Hakikisha kuwa umekuja mahakamani namashahidi wako na wawe tayari kutoa ashahidi wao. Nukuu maswali unayokusudia kuuliza na uyapitie na mashahidi wako kabla ya kesi kusikizwa.
- **Usiwaleta watoto wako mahakamani.** Mahakama

hazina vituo vya kulelea watoto. Watoto hawastahili kuachwa bila kushughulikiwa. Watoto hawatakubaliwa kuwa mahakamani isipokuwa wakati wanahitajika kutoa ushahidi.

- **Subiri hadi hakim/jaji amenena nawe ndiposa uongee.**

Hutubia watu mahakamani ukitumia majina yao ya mwisho na vyeo vyao (kwa mfano, Bwana Kamau, Bi Wanjiku). Katika mahakama za chini, mwite hakim “Mheshimiwa”. Katika mahakama za juu, tumia “Bwana” au “Bi”.

- **Nena ukweli.**